**ENFA Opening Remarks 2025 – Madinatul Bahr on June 9th, 2025**

*Protokoli…*

Ni heshima kubwa kwangu kuzungumza mbele yenu, nyoote mliovaa joho la ushujaa wa elimu.

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuturuzuku neema ya kuiona siku hii ya leo na kutuwezesha kukusanyika hapa kwa ajili ya kutafakari mazuri na yale tunayoyaona ni kizuizi kinachoikabili sekta ya elimu nchini. Nachukua fursa hii pia kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu aubariki mkusanyiko huu kwa Baraka na mafanikio makubwa. AAMIN

Pili, Nachukua fursa hii kuishukuru na kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuandaa mkutano huu, pamoja na kuthamini mchango wa asasi za kiraia (CSOs), katika kuleta ubora wa elimu Zanzibar. Tumepewa heshima ya kushiriki na kuwasilisha neno letu la pamoja mbele ya mkutano huu mkubwa, wa kutathmini maendeleo ya elimu katika taifa letu.

Na nyoote mliopata fursa ya kushiriki mkutano huu, mjitambue kuwa nyinyi ni watu maalum na muhimu sana – hongereni sana!

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

Mada yetu ya mwaka huu, inasema***: "Transforming Education for Sustainable Future: inclusivity, Technology and Resilience".*** Huu ni wito wa kuangalia mustakabali wa elimu yetu kwa makini zaidi. Tumefundishwa kuwa kila changamoto ni fursa iliyojificha! Kwa kupitia changamoto tunazoziibua katika hatua za mchakato wa matayarisho na wakati wa mkutano huu, fursa mbali mbali za mipango, mikakati na utekelezaji wa kupeleka mbele maendeleo ya elimu Zanzibar zinaibuka. Elimu ina uwezo na nguvu kubwa ya kubadilisha maisha. Na hapa naomba nimkumbuke na kumnukuu Jamadari na kiongozi mahiri, aliekuwa Raisi wa Afrika ya Kusini, Bw. Nelson Mandela aliposema wakati wa ziara yake huko Boston, Skuli ya Madison Park High School in, 1990 - "Education is the most powerful weapon we can use to change the world". Mwisho wa kunukuu.

*Ndugu Mgeni Rrasmi,*

Kila mtoto anastahili fursa ya kujifunza na kufaulu. Hii inahitaji sera zinazosaidia, usawa na kushirikisha jamii ili kuhakikisha kila mlengwa anapata nafasi ya kujifunza. Wakati tunafungua milango kwa kila mtoto, tunafungua pia uwezo mkubwa wa maendeleo ya taifa letu.

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

Tukizungumzia Teknolojia—teknolojia ni ufunguo unaoweza kuleta mabadiliko makubwa—kutoa elimu kwa kila pembe, na kuwapa vijana wetu uwezo wa kujifunza kwa njia mpya na za kufurahisha. Tufikirie tutajisikia vipi ikiwa watoto watapewa njia na ufundi wa kujifunza elimu, na hatimaye, kuwa viongozi wa kesho!

Katika zama hizi za kidigitali, Teknolojia, hasa akili bandia (*Artificial Intelligence* au AI), inabeba nafasi muhimu katika kuboresha mfumo wa elimu. AI inaweza kutumika kutoa mafunzo binafsi kwa mwanafunzi, kurahisisha upatikanaji wa elimu kwa maeneo ya mbali, na kuongeza ubunifu na ufanisi wa walimu. Faida ni nyingi na kubwa: kuongeza ubora wa mafunzo, kupunguza upungufu wa rasilimali, na kuwapa vijana uwezo wa kujifunza kwa kasi na ufanisi zaidi. Hii inahakikisha kuwa kila mtoto anapata nafasi ya mafanikio.

Hata hivyo, kama wizara na taifa kwa ujumla, tunapaswa kuwa makini. Matumizi mabaya ya AI—vijana wakiachiwa bila elimu sahihi ya matumizi, au kushindwa kulinda takwimu na taarifa—kunaweza kuongeza mapengo ya kidijitali, kuleta ubaguzi wa kiubunifu, kuongezeka kuporomoka kwa maadili na kusababisha madhara makubwa kwa usalama na faragha za wanafunzi!

Kwa hiyo, hatuwezi kuachwa nyuma. Ni jukumu letu kuhakikisha teknolojia hii inatumika kwa maadili, usalama, na mwelekeo wa maendeleo jumuishi—kwa kufundisha walimu, kuwekeza katika miundombinu na kuhakikisha kila hatua inatoa haki na usawa kwa vijana wa Zanzibar.

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

Maisha hayako kwenye teknolojia pekee—tunahitaji kujenga mifumo imara, inayohimili changamoto za hali ya hewa, magonjwa, au matatizo ya kiuchumi. Elimu ya watoto wetu lazima iweze kuhimili dhoruba na kuwa imara zaidi wakati inapokabiliwa na changamoto!

Na jambo la msingi zaidi—hatuwezi kufanya haya peke yetu. Tunahitaji ushirikiano wa nguvu zote—serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, waalimu, wadau wengine na jamii kwa jumla.

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

Taasisi binafsi za elimu zimejikita vya kutosha katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kutoa elimu bora kwa wote. Naomba nieleze baadhi ya mifano ya juhudi zetu na mikakati endelevu katika kufikia hili…

Juhudi kubwa sana zimejitokeza katika kubeba mzigo wa watoto madarasani kwa kufunguliwa na kuendelezwa zaidi ya skuli binafsi mia nane (800) Zanzibar. Jumuiya ya Skuli Binafsi Zanzibar (ZAPS) inafanya kazi kubwa ikiwemo kutoa elimu kwa watendaji pamoja na kuratibu na kufuatilia mambo yanayohusu skuli binafsi.

Mwanamke Initiative Foundation (MIF), chini ya kauli mbiu " **Developing Skills for Learners for a Sustainable, Innovative, and Inclusive Future**," imewafikia zaidi ya vijana 110 (wanaume 30 na wanawake 80). Mwaka huu, vijana wengine 100 wanatarajiwa kujiunga na mpango huu. Utekelezaji wa programu ya kuwawezesha vijana kupitia elimu ya ujuzi wa kiufundi na teknolojia kwa maendeleo endelevu.

Milele Zanzibar Foundation (MZF) imeleta maendeleo makubwa mwaka uliopita katika kubadilisha elimu kwa njia bunifu. Tumeweza kutumia nguvu ya teknolojia, kuunda maudhui ya kidijitali yanayovutia kwa ajili ya kujifunza mtandaoni na katika maeneo ya mbali, kuwapa walimu mafunzo ya kuwawezesha kutumia maudhui ya sauti katika madarasa yao, kushirikisha wazazi kupitia wasaidizi wa kijamii, na kurusha maudhui ya kielimu kwenye redio. Matokeo yake, tumefikia jumla ya wasikilizaji 272,032—wakiwemo wazazi 181,433, walimu na wanafunzi 90,599—kwa kupitia kurushwa kwa programu zetu za sauti za lugha ya Kiingereza kwenye redio. Aidha, wanafunzi 9,777 (wasichana 5,133 na wavulana 4,644) wamefaidika kutokana na walimu kupatiwa mafunzo ya kuyajumuisha maudhui haya ya sauti kwenye madarasa yao.

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

MZF pia ina furaha kutaja mafanikio ya wanafunzi wetu wa Sekondari wa STEAM. Hii siyo kambi tu bali ni safari ya ubunifu, ubunifu na ugunduzi. Wanafunzi 75 (wakiume 37 na wanawake 38) kutoka skuli 15 walihudhuria *'boot camp'* iliyofanyika Zanzibar. Kati yao, wanafunzi 20 bora (wasichana 10 na wavulana 10), wenye umri wa kati ya miaka 14 hadi 17, pamoja na walimu wanne—wawili wa kiume na wawili wa kike—pamoja na afisa mmoja kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, na nyota wa STEAM (wahitimu na walimu viongozi), waliendelea na safari yao katika *'Boot camp'* Arusha. Huko, walijifunza ujuzi muhimu wa karne ya 21 kama utatuzi wa matatizo, ushirikiano, mawasiliano, na kujitambua, huku pia wakifanya mazoezi ya kuwasilisha mawazo yao kwa ujasiri.

ZRCP imeunda Sera ya Kuendeleza Mabadiliko ya Kidijitali, itakayozinduliwa hivi karibuni. Sera hii inaangazia maeneo muhimu kama vile maendeleo ya ujuzi wa kidijitali na inatoa mfumo kamili wa kuanza kutumia teknolojia ya kielimu (EdTech) kuleta mabadiliko ya kidijitali.

Pamoja na hayo, tumefanya utafiti wa kina kuhusu mfumo anzilishi wa ekologia na kuanzisha kambi na kuandaa kongamano kuchunguza nguvu ya ubunifu wa kidijitali. Utafiti huo pia umelenga jinsi vijana wanavyoweza kutumia teknolojia kuongoza maendeleo ya kidijitali.

Zaidi ya hayo, kupitia Nyota Hub, tumeanzisha mafunzo ya majaribio yanayolenga kuimarisha uwezo wa kutumia AI kwenye uwanja ya elimu. Jitihada hii imeleta mwanga kuhusu njia za kuboresha ujuzi wa kidijitali kwa kuingia kwenye sekta zaidi.

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

Madrasa Early Childhood Program Zanzibar inasukuma mbele maendeleo ya elimu mjumuisho. Kwa miaka mitano iliyopita, kuanzia 2020 hadi 2024, wametekeleza mradi wa kubadilisha elimu kwa kuzingatia ubunifu, unaojikita katika elimu mjumuisho—ndoto iliyotokana na imani kwamba kila mtoto, bila kujali hali alionayo, anastahili kupata elimu bora.

Mradi huu ulikuwa na malengo makuu matatu:

1. Kujenga uwezo kwa wahusika muhimu, hasa walimu wetu,
2. Kuboresha ufikiaji wa elimu bora kwa watoto wote, na
3. Kuweka mkazo wa kipekee kwa watoto wenye ulemavu katika mazingira ya mapema ya kujifunza.

Tunajivunia kutoa taarifa kwamba, mradi umefanikiwa kufikia wilaya tatu—mbili Unguja na moja Pemba. Katika maeneo haya, tumeshirikisha skuli 51, zikiwemo za serikali, binafsi, na za kijamii.

Zaidi ya hayo, mradi umewashirikisha moja kwa moja walimu 813—638 wanawake na 183 wanaume—kuwaandaa kwa maarifa, ujuzi, na zana za kutengenezea mazingira saidizi na jumuishi ya kujifunza.

Idadi hii inaonesha siyo tu matokeo ya kazi, bali pia ni ishara ya kujitolea kwetu kwa usawa, nguvu za kuwashirikisha watu, na imani kuwa elimu ni haki ya wote.

Chama cha Walimu Zanzibar (ZATU) kimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba sera na sheria za elimu zinakuwa shirikishi na jumuishi. Pia zinakuwa ni msaada na nyenzo sahihi za kuongoza usimamizi wa elimu nchini petu. Pia ZATU imekuwa ni jukwaa la kuwaunganisha walimu na kusaidia kutatua changamoto zao ili kuwawezesha kufanya kazi ya kuielimisha jamii pamoja na watoto wetu kwa ufanisi na tija.

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

Ufanisi huu ni ushuhuda wa juhudi za pamoja na ubunifu wa timu zetu mahiri.

Tunajivunia mafanikio haya na tunatarajia kuendeleza kasi hii ili kuhamasisha fikra zaidi za vijana!

Kwa kumalizia, lazima tukubali kuwa, tukifanya kazi kwa umoja na nia njema, tunaweza kuibadilisha Zanzibar kuwa mfano kwa elimu bora, usawa, teknolojia na uhimilivu.

Asanteni sana, na nakutakini mafanikio mema.  - Tuzifanye siku tatu hizi za mkutano huu ziwe za kukumbukwa!